**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Waziri Mkuu**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Butiama**

SHULE YA SEKONDARI KYANYARI


Namba za simu:

Mkuu wa Shule: 0754 962 627 S.L.P 775

Makamu M/Shule: 0782 970 627 Musoma-Mara

Mwalimu wa Malezi: 0766 626 773 kyanyariss@gmail.com


KUMB.NA.JIN/KDT.5/2026/VOL1

Mzazi/Mlezi wa: ………………………………………………

S.L.P ……………………………………………………………

……………………………………………………………

YAH: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA MKOA WA MARA MWAKA 2026**

1.0 Ninayo furaha kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na masomo ya kidato cha tano katika shule hii kwa mwaka wa masomo ………………. na atasoma tahasusi ya **HGK.**

Shule ya sekondari Kyanyari inapatikana wilaya ya Butiama mkoa wa Mara, kwa anayetokea barabara ya Musoma-Mwanza au Mwanza-Musoma ashuke kituo cha Mwibagi Stoo na achukue pikipiki (Bodaboda) hadi shuleni kwa shilingi elfu mbili tu (TZS 2,000.00).

Muhula wa masomo unaanza tarehe…………………… hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe …………….. na mwanafunzi atayeripoti zaidi ya tarehe ……………. hatapokelewa.

2.0 Mwanao atapokelewa shuleni akiwa amekamilisha vitu vifuatavyo:

(i) Nakala (photocopy) ya "**Cheti cha kuzaliwa**" na "**Result slip ya kidato cha nne**" (**Pia vyeti halisi vinahitajika kwa ajili ya uhakiki wakati wa kuandikishwa**)

(ii) Kitambulisho cha **BIMA YA AFYA (Kwa wale wenye BIMA ya afya)**

(iii) Fomu ya Kupimwa Afya (Medical Examination Form) iliyojazwa na Mganga mkuu Hospitali ya serikali.

(iv) Fomu ya kiapo cha Mwanafunzi **ikiwa imejazwa vizuri**.

(v) Fomu ya **Malipo ya Benki** (**Bank Pay Slip**) kwa malipo yote yaliyoanishwa kulipwa katika akunti ya shule.

(vi) Fomu ya utambulisho wa Mwanafunzi (**fomu hii itajazwa shuleni baada ya Mwanafunzi kusajiliwa**).

**Tanbihi**: Mwanafunzi atakuwa amekamilisha usajili wake **pale tu atakapokuwa amekamilisha mahitaji yote** anayopaswa kuja nayo kama yalivyo maelekezo ya fomu hii.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI**

HEADMASTER
KYANYARI SEC. SCHOOL
B*X 77* M*SOMA

**Guka Dioniz**

MKUU WA SHULE

### 3.0 MAHITAJI MAALUM YA KUZINGATIA

### 3.1 SARE ZA SHULE

(i) Suruali mbili (2) **Nyeusi** zisizobana na **zinazogusa visigino (siyo modo).**

(ii) Suruali mbili (2) **Kijivu** kwa ajili ya shamba dress.

(iii) Shati **Nyeupe** mbili (2) mikono mirefu zenye nembo ya shule na tai ndefu mbili (2) nyeusi. (**Tai zinapatikana shuleni kwa Tsh.5,000 kwa kila moja**)kwa atakayehitaji

(iv) T-shirt mbili (2) za shule zenye nembo ya shule (**Zinapatikana shuleni kwa TZS 15,000.00 kila moja**) kwa atakayehitaji

(v) Track suit moja (1) **Nyeusi.**

(vi) Jezi ya michezo (Bukta na Fulana)moja (1) **Bluu Bahari.**

(vii) Sweta **rangi ya bluu** mikono mirefu lenye shingo ya **V**

(viii) Soksi jozi mbili (2) **Nyeusi.**

(ix) Mkanda **Mweusi** wa ngozi wa kuvalia suruali.

(x) Viatu jozi mbili (2) **Vyeusi** vya kufunga na kamba vyenye kisigino kifupi.

(xi) Viatu vya michezo angalau jozi moja (1).

### 3.2 VIFAA VYA USAFI

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na vifaa vya usafi vifuatavyo: Soft broom moja (1), squeezer moja (1), sabuni ya maji ya kusafishia chooni lita 5, na jembe lenye mpini moja(1)

### 3.3 MAHITAJI TA TAALUMA

Kila mwanafunzi anatakiwa kuja na **Ream A4 (Double A/bright white multipurpose office paper)** mbili (2) kwa mwaka mzima kwa ajili ya mitihani na mazoezi mbalimbali. Mwanafunzi atakayeleta aina tofauti ya Ream tajwa hazitapokelewa.

### 3.4 MICHANGO MBALIMBALI

Kila mwanafunzi atatakiwa kutoa kiasi cha shilingi elfu themanini (TZS 80,000.00) kwa mchanganuo ufuatao kwenye jedwani:

| Na | AINA YA MCHANGO | KIASI (TZS) |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000.00 |
| 2 | Tahadhari | 5,000.00 |
| 3 | Nembo | 5,000.00 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000.00 |
| **JUMLA** | | **80,000.00** |

Malipo yote tajwa hapo kwenye jedwari yalipwe kwenye Akaunti ya shule.

Namba ya Akaunti: **30301200359**

Jina la Akauntii: **KYANYARI SECONDARY SCHOOL**

Jina la Benki: **NMB**

**Zingatia:** Hakikisha ufanyapo malipo majina kamili ya mwanafunzi yameandikwa kwenye Bank pay slip itayayokabidhiwa kwa mhasibu wa shule mara tu baada ya kuripoti shuleni.

**3.5 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI**

(i) Godoro lenye ukubwa wa $2\frac{1}{2}$kwa 6.

(ii) Tranka moja.

(iii) Mashuka ya **Bluu** jozi mbili (2), mto (1), chandarua cha pink (1)

(iv) Taulo, **vest nyeupe,** na nguo za ndani za kutosha.

(v) Ndoo ndogo ya lita kumi moja (1) na Kidumu cha lita 5 kwa ajili ya maji ya kunywa

(vi) Kandambili kwa ajili ya kuogea

(vii) Sabuni ya kuogea na kufulia, miswaki na dawa ya meno.

(viii) Vyombo vya chakula (Sahani, bakuli, kijiko na kikombe). **(Vyombo vya chakula visiwe vya bati).**

**3.6 MAHITAJI BINAFSI YA MWANAFUNZI DARASANI**

(i) Vitabu vya masomo ya tahasusi aliyochaguliwa **(Orodha ya vitabu imeambatanishwa).**

(ii) Madaftari 10 (Counter Books 3 au 4 Quires), Mathematical set (1), Scientific calculator (1), penseli za kutosha, rula, kalamu nyeusi au bluU za kutosha, A4 graph paper pads mbili (2) na begi la kubebea daftari darasani rangi nyeusi (1).

**3.7 BIMA YA AFYA**

Mzazi inatakiwa umkatie mwanao Bima ya Afya anaporipoti shuleni aje nayo. Kama ukishindwa kumkatia basi wakati wa kuripoti shuleni aje na Bank Pay Slip ya kiasi cha shilingi hamsini elfu mia nne (TSZ 50,400.00) kwa mwaka ili akatiwe Bima shuleni.

Namba ya Akaunti: **30301200359**

Jina la Akauntii: **KYANYARI SECONDARY SCHOOL**

Jina la Benki: **NMB**

**4.0 SHERIA, KANUNI NA TARATIBU MUHIMU ZA SHULE**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu na Ofisi ya Rais-TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na:

**4.1 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE**

Sheria na kanuni hizi zinazingatia misingi ya HESHIMA, ADABU, UAMINIFU, UTII na TABIA NJEMA kwa ujumla. Mwanafunzi anatazamiwa kuwa mfano mzuri kwa heshima, tabia na vitendo; hivyo ni pamoja na:

(i) Mwanafunzi atasimama anapomsalimu mwalimu, mtumishi wa shule asiye mwalimu au mtu yeyote aliyemzidi umri.

(ii) Hairuhusiwi kwa mwanafunzi kutumia lugha chafu au ya kihuni popote na wakati wowote hata kwa wanafunzi wenzake.

(iii) Hairusiwi kwa mwanafunzi;

(a) Kufuga kucha na nywele

(b) Kufuga ndevu

(c) Kunyoa kipara au mtindo wa kihuni

(d) Kutukana

(e) Kutia dawa nywele (curly) na kujichubua ngozi ya mwili kwa madawa

(f) Kuvaa vitu kama mapambo mfano heleni, mikufu, bangili, kacha au vitu vya kiimani.

(g) Kofia, kanzu, vilemba, suruali fupi kwa kuwa shule hii ni ya **serikali**

(h) Kuvaa viatu vya soli nene na ndefu

(i) Kuvaa kaptura na kandambili kwenye Bwalo la chakula na Ofisi zote za shule

(j) Kuvaa suruali chini ya kiuno yaani mtepesho

(k) Kuvaa nguo za mtindo, mfano model

(iv) Anatakiwa kuwa mtulivu asipige kelele au vitendo vyovyote vitakavyo sababisha usumbufu kwa wengine anapokuwa darasani, maktaba, bwenini, wakati wa kujisomea (prep) na katika mikusanyiko yoyote mfano paredi n.k.

(v) Mwanafunzi **LAZIMA** awahi na ahudhurie mahali anapotakiwa katika shughuli za shule. Hivyo Mwanafunzi:

(a) Aripoti shueni tarehe ya kufungua shule na kujiandikisha rasmi siku na saa ya kuripoti kwa mwalimu anayehusika.

(b) Ahudhurie vipindi vyote darasani kama ilivyopangwa.

(c) Ahudhurie kwenye kazi atakazopangiwa.

(d) Ahudhurie kwenye paredi ya uhakiki uwepo wake shuleni (Rollcall), Ukaguzi wa usafi, kupandisha Bendera ya Taifa na paredi ya kawaida.

(vi) **NI LAZIMA** Mwanafunzi awe katika sare ya shule na awe na **KITAMBULISHO** cha shule nyakati zote awapo shuleni na nje ya shule kama: - Anapotoka nje ya shule kwa ruhusa maalumu kwenda Posta, Kanisani, Msikitini, Hospitali, Benki, likizo au kwa shughuli yoyote itakayomlazimu kwenda nje ya shule.

(vii) Mwanafunzi lazima ahudhurie prep inayoanza saa 2:00 usiku hadi saa 4:30 usiku, mwanafunzi awe kitandani kwake wakati wa kuzima taa (light out) saa 4:45 usiku.

(viii) Mwanafunzi haruhusiwi kutumia umeme kwa shughuli yoyote ile awapo bwenini au darasani isipo kuwa kuwasha taa tu.

(ix) **Hairuhusiwi** kufanya mikutano au vikao yoyote/vyovyote shuleni pasipo kibali cha Mkuu wa Shule na ikiwa kibali kimetolewa kikundi au chama kitatakiwa kuandika muhtasari wa kikao na nakala kuwasilishwa kwa Mkuu wa Shule.

(x) Mwanafunzi anawajibika kuwa msafi wa mavazi na mwili wake na kushiriki kuyaweka mazingira ya shule katika hari ya usafi wakati wote.

(xi) Mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ya Shule ya sekondari Kyanyari muda wote akiwa ndani na nje ya shule na achomekee shati lake. **Mavazi yasiyo sare ya shule hayaruhusiwi kabisa**.

(xii) Mwanafunzi haruhusiwi kujihusisha na masuala ya siasa katika kipindi chote awapo mwanafunzi.

### 4.2 MAENEO YASIYORUHUSIWA

Mwanafunzi haruhusiwi kufika/kuingia sehemu zifuatazo bila ruhusa maalumu:

(i) Ofisi za shule

(ii) Bohari za shule

(iii) Kwenye disko, ngoma, muziki au kwenye sherehe yoyote ndani na nje ya shule

(iv) Maabara

(v) Baa, klabuni, au mahali popote panapouzwa pombe au vileo vingine

(vi) Nyumba za wageni (Guest House au Lodge)

(vii) Nyumba za watumishi/walimu.

### 4.3 MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

(i) Wizi

(ii) Uasherati, ushoga, ulawiti na ubakaji

(iii) Ulevi wa aina yeyote kama utumiaji wa madawa ya kulevya, pombe, sigara, bangi, ugoro, mirungi n.k

(iv) Makosa ya jinai

(v) Kuoa

(vi) Kusababisha mimba

(vii) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

(viii) Kupigana au kumpiga mwingine

(ix) Kudharau Bendera ya Taifa

(x) Kulala nje ya shule bila ruhusa ya Mkuu wa Shule

(xi) Kuchochea au kufanya vurugu, kugoma kwa namna yeyote

(xii) Kutumia lugha ya matusi

(xiii) Kumdharau kiranja wa shule, mwalimu, mfanyakazi wa shule asiye mwalimu na jamii kwa ujumla

(xiv) Kutohudhuria vipindi darasani au kutofanya mazoezi ya darasani, majaribio na mitihani kwa makusudi

(xv) Mwanafunzi kumiliki simu au sehemu ya simu kama vile laini ya simu, charger n.k

(xvi) Mwanafunzi kumiliki kifaa chochote cha umeme kama vile pasi, heater n.k

(xvii) Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa aina yeyote bila idhini ya daktari au Mkuu wa Shule.

(xviii) Kufanya jaribio la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

**MUHIMU:**

(a) **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu, laini ya simu wala kifaa chochote chenye kutumia umeme kwa namna yeyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu wala laini ya simu ya mwanafunzi;**

(b) **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake (Kwahiyo kitanda kimoja kitatumiwa na mwanafunzi mmoja tu) au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa.**

(c) **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum kutoka kwa Mkuu wa Shule. (Kwa changamoto ya msiba au ugonjwa).**

(d) **Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi (sms) au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yupo mahututi, hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO TAARIFA YOYOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO:**

**(i) Mkuu wa Shule: 0754 962 627**

**(ii) Makamu Mkuu wa Shule: 0782 970 627**

**(iii) Mwalimu wa Malezi (Patroni): 0766 626 773**

5.0 Tafadhari soma kwa makini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**Ofisi ya Waziri Mkuu**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**
**Halmashauri ya Wilaya ya Butiama**
SHULE YA SEKONDARI KYANYARI

Namba za simu:

Mkuu wa Shule: 0754 962 627
Makamu M/Shule: 0782 970 627
Mwalimu wa Malezi: 0766 626 773

S.L.P 775
Musoma-Mara
kyanyariss@gmail.com

## FOMU YA UTAMBULISHO WA MWANAFUNZI

1. Jina la Mwanafunzi ------------------------------------------------------------------------
2. Tarehe ya kuzaliwa ---------------------- Dini -------------------- Dhehebu -------------------
3. Mkoa unaoishi ---------------- Wilaya--------------- Kata---------------Mtaa/kijiji -------------
4. Jina la Shule ulipohitimu kidato cha IV ------------------------------ Mwaka ------------
5. Namba yako ya mtihani wa kidato cha nne ---------------------------------------------
6. Kidato unachokuja kujiunga hapa shule ya sekondari Kyanyari ---------------------------
7. Taarifa za wazazi/ndugu zako (Mfano Baba, Mama, Mjomba, Dada, Kaka, Shangazi n.k) wa karibu wanaokufahamu na wanaweza kutoa taarifa zako za kina zitakapohitajika. Pia hawa ndio ndugu pekee watakaoruhusiwa kukutembelea shuleni wakati wote uwapo shuleni.

| Na | JINA KAMILI | UHUSIANO | KAZI | ELIMU | ANUANI | SIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | | | | | | |
| 2 | | | | | | |
| 3 | | | | | | |
| 4 | | | | | | |
| 5 | | | | | | |

Picha (Passport size) zenye rangi ya kitambaa cha blue nyuma za wazazi au ndugu wenye majina kwenye jedwari hapo juu zibandikwe hapa chini kwa mfuatano jinsi majina yalivyoandikwa.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Passport 1 | Passport 2 | Passport 3 | Passport 4 | Passport 5 |

Ninathibitisha/Ninaapa kwamba taarifa zote zilizotolewa hapo juu ni kweli kadili ya uelewa wangu.

Saini ya mwanafunzi: --------------------------- Tarehe: ------------------------

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**Prime Minister's Office**

**Regional Administration and Local Government**

**Butiama District Council**

KYANYARI SECONDARY SCHOOL

Contacts:

The Head of School: 0754 962 627 P.O BOX 775

Second Master: 0782 970 627 Musoma-Mara

Patron: 0766 626 773 kyanyariss@gmail.com

## MEDICAL EXAMINATION FORM

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION FOR---------------------------------------- FORM V ------------- (Year)

Please examine the above named as to his/her fitness to school as a student.

Name and signature of requesting Officer.

Name ------------------------------------------ Signature ----------------------------

Date ---------------------------------

To be completed by a Government Medical Officer in respect of FORM 5 entrants.

Student's Full Name ------------------------------------------------------------------------

Age/Years ---------------------------------------- Sex (M/F) ----------------------------

Blood count (Red and White) ---------------------------------------------------------

Stool Examination ---------------------------------------------------------------------

Urinalysis -----------------------------------------------------------------------------

Syphilis Test -------------------------------------------------------------------------

T.B Test ------------------------------------------------------------------------------

Eye Test ------------------------------------------------------------------------------

Ears Test -----------------------------------------------------------------------------

Chest ---------------------------------------------------------------------------------

Spleen --------------------------------------------------------------------------------

Abdomen -----------------------------------------------------------------------------

Blood Group -------------------------------------------------------------------------

ADDITIONAL INFORMATION: e.g. Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases etc.

-----------------------------------------------------------------------------------------

-----------------------------------------------------------------------------------------

I have examined the above named and I consider that he/she is physically fit/unfit to pursue further studies.

Name and Signature of Certifying Officer

Name ------------------------------------------ Signature ----------------------------

Station ------------------------------------------ Designation ----------------------------

Date ------------------------------------------ Stamp ----------------------------

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Waziri Mkuu**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Butiama**

SHULE YA SEKONDARI KYANYARI

Namba za simu:

| | |
|---|---|
| Mkuu wa Shule: 0754 962 627 | S.L.P 775 |
| Makamu M/Shule: 0782 970 627 | Musoma-Mara |
| Mwalimu wa Malezi: 0766 626 773 | kyanyariss@gmail.com |


YAH: **AHADI/KIAPO CHA MWANAFUNZI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KYANYARI**

Mimi------------------------------------------------------------------------------------------------- Kidato cha V tahasusi ya ---------- ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI KYANYARI KIDATO CHA TANO** mwaka wa masomo 2026/2027 ninapokea na kukubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na shule ya Sekondari Kyanyari.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu hivyo ninaahidi kuitumia nafasi hii kwa kujituma na kusoma kwa bidii na kuwa na mwenendo mwema wakati wote kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania na kwa ajili yangu pia.

Ninaamini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudi haya ni hujuma kwa Taifa langu, shule ya Sekondari Kyanyari, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni:

(i) Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
(ii) Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
(iii) Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu wala kushawishi au kuchochea migomo.
(iv) Niwapo mwanafunzi sitajishughulisha na masuala ya siasa katika chama chochote cha siasa.
(v) Ikiwa nitakiuka sheria, kanuni na taratibu za shule kama nilivyozisoma na kuzielewa, basi nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/mlezi wangu---------------------------------------- (Jina la mzazi/mlezi) namba ya simu------------------------------------------ kwa ajili ya hatua zaidi.

Saini ya mwanafunzi------------------------------------------- Tarehe----------------------------

Jina la mzazi/mlezi------------------------------------------- Tarehe ----------------------------

Saini ya mzazi/mlezi ----------------------------------------------

Jina la Mkuu wa Shule ------------------------------------ Tarehe -----------------------------

Saini ya Mkuu wa Shule -----------------------------------

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Waziri Mkuu**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Butiama**

SHULE YA SEKONDARI KYANYARI


Namba za simu:

Mkuu wa Shule: 0754 962 627 S.L.P 775

Makamu M/Shule: 0782 970 627 Musoma-Mara

Mwalimu wa Malezi: 0766 626 773 kyanyariss@gmail.com


YAH: **TAMKO LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI**

Mimi------------------------------------------------- mzazi/mlezi wa ------------------------------ ninakubali mtoto wangu kupata na kupokea nafasi ya kujiunga na shule hii. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule wakati wote kuhakikisha mwanangu anatekeleza wajibu kwa Taifa na shule, ikiwa ni pamoja na kuheshimu na kufuata sheria, kanuni na taratibu zote za shule pamoja na kuhakikisha anasoma kwa bidii ili kufanya vizuri katika masomo yake. Pia ninaahidi kutoa mahitaji yote kwa mwanangu kila nitakapohitajika kufanya hivyo.

Anuani yangu ya kudumu ni: ------------------------------------------------

------------------------------------------------

Namba ya simu: ------------------------------

Saini ya mzazi/mlezi: ----------------------------- Tarehe: -------------------

Jina la Mkuu wa Shule: -------------------------- Tarehe: --------------------

Saini ya Mkuu wa Shule: ---------------------

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**Ofisi ya Waziri Mkuu**

**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa**

**Halmashauri ya Wilaya ya Butiama**

SHULE YA SEKONDARI KYANYARI

Namba za simu:

Mkuu wa Shule: 0754 962 627 S.L.P 775

Makamu M/Shule: 0782 970 627 Musoma-Mara

Mwalimu wa Malezi: 0766 626 773 kyanyariss@gmail.com

**ORODHA ZA REJEA YA VITABU KWA KILA MWANAFUNZI**

Mwanafunzi anaweza kununua baadhi ya rejea ya vitabu vifuatavyo kama vilivyopendekezwa na shule kulingana na uhitaji wa muhtasari wa somo husika.

## 1. HISTORY

(i) Tanzania Institute of Education (2024). ***History for Advanced Secondary Schools, student's book form five.*** (Revised edition). Tanzania Institute of Education.

(ii) Tanzania Institute of Education (2024). ***History for Advanced Secondary Schools, student's book form six.*** (Revised edition). Tanzania Institute of Education.

(iii) Yassin, S. (2024). ***Essentials in Advanced Level History Paper 1.*** (Revised edition). Ahmadiyya Printing Press.

(iv) Yassin, S. (2024). ***Essentials in Advanced Level History Paper 2.*** (Revised edition). Ahmadiyya Printing Press.

## 2. GEOGRAPHY

(i) Burnet, R.B. (2008). ***Physical Geography in Diagrams for Africa***. Pearson Education Limited.

(ii) Maganga, J.P. (2019). ***Practical Geography; Principles and Practice for A-level***. Juma P. Maganga.

(iii) Msabila, D.T. (2014). ***A Comprehensive Approach to Physical Geography, for secondary schools***. Dar es Salaam.

(iv) Pritchard, J.M. (1990). ***Practical geography for Africa***. Longman Group Ltd.

(v) Pritchard, J.M. (1984). ***Practical geography for Africa***. UK Limited.

(vi) Tanzania Institute of Education (2024). ***Physical Geography for Advanced Secondary Schools, student's book form five and six.*** (Revised edition). Tanzania Institute of Education.

*(vii)* Tanzania Institute of Education (2024). ***Practical Geography for Advanced Secondary Schools, student's book form five and six.*** (Revised edition). Tanzania Institute of Education.

## 3. KISWAHILI

(i) Kihore, Y.N., Massamba, D.P.B & Msanijila, Y.P. (2003). ***Sarufi maumbo ya Kiswahili sanifu: (SAMAKISA) Sekondari na Vyuo.*** TUKI.

(ii) Kihore, Y.N., Massamba, D.P.B & Msanijila, Y.P. (2003). ***Sarufi miundo ya Kiswahili sanifu: (SAMAKISA) Sekondari na vyuo.*** TUKI.

(iii) Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). ***Kiwahili Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Lugha na Sarufi***. Taasisi ya Elimu Tanzania.

(iv) Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). ***Kiwahili Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Fasihi***. Taasisi ya Elimu Tanzania.

(v) Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2002***). Nadharia ya Lugha ya Kiswahili, Kidato cha 5 na 6.*** Aroplus Industries Ltd.

(vi) Nkwera, Fr. F. V. (2003). ***Sarufi, Fasihi na Uandishi wa Vitabu, Sekondari na Vyuo***. Creative Prints Ltd.

(vii) Maganga (1997). ***OSW 102: Historia ya Kiswahili***. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

(viii) Masebo, J. A. & Nyangwine, N. (2011). ***Nadharia ya fasihi: Kiswahili 2: Kidato cha 5 na 6: fasihi kwa ujumla***. Nyambari Nyangwine Publisher.

(ix) Wanjala, F. S. (2011). ***Misingi ya Ukalimani na Tafsiri kwa shule, vyuo na Ndaki***. Serengeti Educational Publishers (T) LTD.

(x) TUKI. (2004). ***Kamusi ya Kiswahili Sanifu***. (2nd ed.). Oxford University Press.

**4. ACADEMIC COMMUNICATION SKILLS**

(i) Tanzania Institute of Education (2024). ***Academic Communication for Advanced Secondary Schools, student's book form five***. Tanzania Institute of Education.

(ii) Tanzania Institute of Education (2024). ***Academic Communication for Advanced Secondary Schools, student's book form six***. Tanzania Institute of Education.

**5. HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

(i) Taasisi ya Elimu Tanzania (2024). ***Historia ya Tanzania na Maadili Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano***. Taasisi ya Elimu Tanzania.

(ii) Taasisi ya Elimu Tanzania (2024). ***Historia ya Tanzania na Maadili Shule za Sekondari, Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Sita***. Taasisi ya Elimu Tanzania.